



Baadhi ya ukweli muhimu kuhusu ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19)



UNAWEZA kupona ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).

Kupata ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) haimaanishi utakuwa nao kwa maisha yote. Watu wengi ambao wanapata COVID-19 huona na virusi kutoka katika miili yao. Ikiwa utapata ugonjwa, hakikisha unatibu dalili zako. Ikiwa una kikohozi, homa, na shida ya kupumua, tafuta huduma ya matibabu mapema - lakini piga simu kituo chako cha afya kwanza. Wagonjwa wengi huona baada ya uangalizi.




Ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) hauathiri tu watu wazee –unaathiri watu wa rika zote.

Watu wazee na watu wenye uhitaji wa matibabu kama vile wagonjwa wa moyo, pumu, ugonjwa wa kisukari, na shinikizo la damu huonekana kuwa katika hatari kubwa ya kuathiriwa sana na ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19). Shirika la Afya Ulimwenguni linashauri watu wa rika zote kujikinga na virusi, kwa mfano, kuzingatia usafi mzuri wa mikono na usafi katika kupumua.



Unahitaji kukaa na mtu mwenye maambukizi kwa dakika 10 ili kupata maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19).

Hii ni UONGO. Inawezekana kuambukizwa kwa muda mfupi au kupata virusi kutoka kwa nyuso za vitu vilivyo dondokewa na virusi.



Wakati maji safi hayapatikani, maji chafu kidogo yanafaa dhidi ya ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) kama utatumia sabuni wakati wa kuosha mikono yako.